

HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

TAARIFA YA CHANJO YA MBWA 2016

Halmashauri ya wilaya ya Iringa huchanja mbwa na paka kila mwaka kuzuia ugonjwa hatari wa kichaa cha mbwa kwa binadamu na kwa wanyama wengine wenye damu moto kwa njia ya kampeni (Mass vaccination).

Kampeni ya kichaa cha mbwa huhusisha uhamasishaji na utoaji elimu kwa jamii, utoaji wa chanjo kwa mbwa, ufuatiliaji wa mbwa wasiochanjwa na kuua mbwa wazururaji (Stray dogs).

Katika mwaka wa 2016 Kampeni ya chanjo ya kichaa cha mbwa ilifanyika katika kipindi cha Julai hadi Oktoba katika maeneo yote ya Halmashauri. Matokeo ya zoezi hili ni kama ifuatavyo;

a) Uhamasishaji na utoaji elimu kwa jamii;

Katika kampeni ya mwaka huu, uhamasishaji na utoaji wa elimu umefanywa na wataalamu wa mifugo kwa kushirikiana na wataalamu wa afya walioko ngazi kata na vijijini.

b) Utoaji wa chanjo;

Katika kipindi hiki jumla ya mbwa 12,778 walipata chanjo ya kuzuia ugonjwa wa kichaa cha mbwa kati ya 13,223. Idadi hii ni sawa na asilimia 96.6%, aidha jitihada zinaendelea kuwadhibiti wamiliki wa mbwa pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria na kuua mbwa wote wazuraji vijiji wasiokuwa na umiliki.

c) Ufuatiliaji wa mbwa wasiochanjwa;

Baada ya kukamilisha kwa zoezi la uchanjaji, ufuatiliaji wa mbwa ambao hawakupata chanjo ulifanyika na wenye mbwa kuchukuliwa hatua na watendaji wa vijiji na kata. Pamoja na kuchukuliwa hatua, wamiliki walilazimika kuwapeleka mbwa wao kupata chanjo.

d) Kuua mbwa wazururaji (wasio na wamiliki);

Jumla ya mbwa 123 waliuawa na wananchi kwa kutumia silaha mbalimbali pamoja na sumu. Idadi hii inajumuisha mbwa walioonyesha dalili za ugonjwa. Kampeni ya kuuwa mbwa wazururaji haikufanyika kutokana na ukosefu wa fedha.

Changamoto

- Elimu ndogo kwa wafugaji kuhusu ugonjwa na umuhimu wa chanjo
- Kutozingatia ufugaji bora wa mbwa ambao husababisha mbwa kuuma watu na wao kupata maambukizi ya kichaa kwa urahisi.
- Ukosefu wa fedha za kununulia risasi au sumu na kuendeshea kampeni ya kuuwa mbwa.

Ufumbuzi

- Kutoa elimu juu ya ugonjwa wa kichaa cha mbwa na umuhimu wa chanjo, ufugaji bora wa mbwa kwa wafugaji ikiwa ni pamoja na kuwalisha, kuwajengea sehemu ya kuishi na kuwapa matibabu stahiki.
- Halmashauri za vijiji kwa kushirikiana na wataalam wa ugani kuwatambua mbwa wasiokuwa na mmiliki ili hatua sitahiki zichukuliwe.
- Kuchukua hautua za kisheria kwa wamiliki ambao hawajachanja na wanaoacha mbwa kuzurura nyakati za mchana.
- Wananchi kuzingatia taratibu za ufugaji wa mbwa ambapo hutakiwa kuwafungia kuanzia saa 11.00 asubuhi na kufunguliwa saa 4.00 usiku.
- Halmashauri imetunga sheria ndogo ya kudhibiti magonjwa ya mlipuko ya mifugo na bado kuidhinishwa na TAMISEMI.

TAARIFA YA CHANJO YA MBWA DHIDI YA KICHAA KWA MWAKA 2016

S/N	KATA	IDADI YA MBWA TARAJIWA KUCHANJWA	MBWA WALIOCHANJWA	MBWA WALIOUJWA
1	Kising'a	713	722	2
2	Kihorogota	401	395	4
3	Malengamakali	789	817	6
4	Izazi	332	358	7
5	Migoli	492	506	6
6	Itunundu	223	198	9

7	Ilolompya	192	189	5
8	Mlenge	206	210	5
9	Idodi	359	356	11
10	Mahuninga	402	352	4
11	Mlowa	536	524	11
12	Maboga	298	281	5
13	kihanga	201	187	2
14	Wasa	261	257	3
15	Ifunda	461	467	2
16	Kalenga	381	376	3
17	Kiwere	602	610	2
18	Nzihi	556	525	3
19	Magulilwa	791	797	1
20	Luhota	1087	1,138	2
21	Lyamgungwe	563	558	3
22	Mgama	485	492	5
23	Mseke	545	539	6
24	Masaka	241	234	1
25	Nyang'olo	577	563	5
26	Lumuli	353	317	3
27	Ulanda	792	781	4
28	Mboliboli	384	346	3
		13,223	12,778	123